Sabato

“Muumbaji mkarimu, baada ya siku sita za Uumbaji, alipumzika siku ya saba na akaanzisha Sabato kwa ajili ya watu wote kama ukumbusho wa Uumbaji. Amri ya nne ya sheria za Mungu zisizobadilika inaagiza kuadhimishwa kwa Sabato hii ya siku ya saba kama siku ya mapumziko, ibada, na huduma kulingana na mafundisho na uzoefu wa Yesu, Bwana wa Sabato. Sabato ni siku ya kushirikiana kwa furaha na Mungu na sisi kwa sisi. Ni mfano wa ukombozi wetu katika Kristo ishara ya utakaso, ishara ya utii wetu, na mwonjo wa umilele wetu katika ufalme wa Mungu. Sabato ni ishara ya daima ya agano la milele la Mungu kati yake na watu wake. Kuutunza kwa furaha wakati huu mtakatifu toka jioni hadi jioni, jua kuchwa hadi jua kucha, ni adhimisho la matendo ya Mungu ya uumbaji na ukombozi.” (Mwa. 2:1-3; Kut.20:8-10; Luk. 4:16; Isa. 56:5, 6; 58:13, 14; Mat. 12:1-12; Kut. 31:13-17; Eze.20:12, 20; Kumb. 5:12-15; Ebr.4:1-11; Wal. 23:32; Mk. 1:32)

Mara baada ya uumbaji, Adam na Hawa walisherehekea sabato ya kwanza Mw. 1:31 Mw. 2:1- 3. Sabato imejaa kwenye Biblia yote. Hata hivyo kwa ajili ya somo la leo, tutaangalia Edeni, Sinai, Agano, Kristo na Sabato, Sabato na Mitume/Wanafunzi pia tutamalizia na Umuhimu wa Sabato kiroho.

Sabato Edeni Mw. 2:1 -3
Mungu alivyosherehekea sabato ya kwanza
Akaibariki – Akaipa upendeleo wa kipekee wa kimbingu
Akastarehe – Akaacha kufanya kazi
Akaitakasa – Akaitenga kwa makusudi matakatifu
Maelezo kwa ajili ya Adamu na Hawa ni kwamba baada ya kuumbwa, waliingia katika raha pamoja na Mungu. Badala ya kuanza kazi, walipata nafasi ya kuwa na Mungu katika kustarehe kwake.

Sinai
(i) Mwezi moja kabla ya kutangaza sheria, Mungu aliahidi ulinzi dhidi ya maradhi kwa wanaotii amri zake (Kut. 15:26 cf Mw. 26:5) Baadaye akawapa mana kwa utaratibu wa kujali sabato, (Kut. 16:2, 16 - 19, 23 -24). Kwa miaka 40, zaidi ya sabato 2,000, kumbukumbu iliwekwa kwenye akili za Wana wa Israeli juu ya sabato.

(ii) Sabato ilitamkwa kuwa mojawapo ya amri 10 za Mungu Kut. 20:8-11. Msisitizo ukiwa Mungu ndiye mmiliki wa mbingu na nchi, kama muhuri kuwa ni Mtawala wa ulimwengu.

Agano
Sheria ya Mungu iliwekwa kama agano, Sabato nayo imetamkwa kuwa ni agano. (Kut. 34:27, Kut. 31:17, 13). Sheria imewekwa kuonyesha upendo, (Kumb. 7: 7, 8), Sabato nayo huonyesha upendo wetu kwa Mungu.

Sabato na Kristo

Yesu ni mwumbaji na mkombozi (Yoh. 1:3 Kol. 1:16; Yoh. 3:16)Hivyo alipomaliza kazi alipumzika Mw. 2: 1- 3. Alipoishi na wanadamu, Yesu aliiheshimu Sabato (Luka 4:16, Ebr. 13:8). Alifundisha kuwa Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu (Mk. 2: 27). Yeye ndiye aliyeiumba na kuitetea (Mk. 2: 28, Yoh. 5: 17). Alipofikia mwisho wa huduma yake duniani, akionya juu ya hatari itakayowakuta watu wa Mungu, aliwakumbusha kuomba kuwa kukimbia kwao kusiwe siku ya Sabato (Mt. 24:20). Alipokufa siku ya Maandalio (Luka 23:54) alitamka kuwa imekwisha (Yoh. 19:30) na kupumzika siku ya sabato baada ya kukamilisha kumkomboa mwanadamu. (Luka 23:56).

Wanafunzi / Mitume na Sabato

Wanafunzi / mitume waliiheshimu sana Sabato. Kwa kuwa Yesu alikufa siku moja kabla ya Sabato, taratibu za mazishi yake ziliingiliwa na Sabato. Luk. 23:54-56, Luk. 24:1. Kama Kristo alivyofundisha siku ya Sabato, ndivyo walivyofanya wanafunzi.

Walihudhuria ibada siku ya Sabato Mdo. 13:14, Mdo. 17: 1, 2, Mdo. 18:4

Hata mataifa walialika mitume wahubiri siku ya Sabato Mdo. 13: 42, 44

Kuna wakati walikosa mahali pa kuabudu, wakalazimika kusali mahali walipoona panafaa Mdo. 16:13. Hivyo ndivyo utume wa Paulo ulivyoiona siku ya sabato.

Ijulikane kuwa ibada ya siku ya Sabato ni tofauti na sikukuu za taifa la kiyahudi ambazo nazo zilijulikana kama sabato (Law. 23). Paulo alizipinga sikukuu hizo (Kol.2:16; Gal.4:10, 11.) Ikumbukwe kuwa hizo zilitolewa kama nyongeza Law. 23: 37, 38)

Wengine wanadhani kuwa siku ya Bwana ya Uf. 1: 10 kuwa ni siku ya Jumapili. Ni kweli ipo siku ya Bwana ya aina tofauti katika Biblia (Mal. 4: 1, 5) Hata hivyo, kuna msisitizo kuwa siku ya Bwana ni siku ya Sabato. (Kut. 20: 10, Isa. 58: 13, Mk. 2: 28.)

Ni makusudi ya Mungu kuwa wote watakaomwabudu katika mbingu mpya na nchi mpya waabudu siku ya Sabato. Isa. 66: 22, 23.

Umuhimu wa Sabato kiroho

1. Ni ukumbusho wa Uumbaji (Kut. 20. 11)
   Kama Sabato ingaliheshimiwa kadiri ya madai ya amri ya nne, kusingekuwako makafiri, wanaoona shaka kuhusu Mungu na waabudu sanamu.
2. Ni ishara ya kukombolewa (Kumb. 5: 15)
3. Ni ishara ya kutakaswa (Kut. 31: 13, Ez. 20:20)
4. Ni ishara ya utii wetu kwa Mungu (Uf. 14:12, 9)
5. Ni wakati wa ushirika (Mw. 1: 24, 25, Kut. 20: 10)
6. Ni ishara ya kuokolewa kwa imani Mt. 11: 28, 29. Mataifa wengine wanaweza kutii amri za Mungu kwa kadiri ya ufahamu wao, (Rum. 2: 14-16) lakini kwa wakristo, sabato inatupa kutambua kwamba ukombozi wetu siyo kwa juhudi zetu bali ni ni kwa neema ya Mungu tu.
7. Ni ishara ya kupumzika katika Kristo (Ebr. 4: 4, 9, 10)

Mabadiliko ya Sabato
Kwa kuwa sabato ina umuhimu katika kumtambua na kumwabudu Mungu, haishangazi kuona Shetani ameipiga vita kwa ukali wote.

Nani atakuwa amebadili sabato? Jamii kubwa ya Wakristo husali siku ya kwanza ya juma badala ya siku ya saba. Hii inafanya kuwa na swali, je ni nani atakuwa amebadili sabato?

Je ni Mungu? Mungu anasema "Mimi sitalihalifu agano langu, sitalibadili neno lililotoka midomoni mwangu. (Zab. 89: 34). "Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeu geu." (Malaki 3:6). Mtunga Zaburi asema "Maagizo yake yote ni amini, Yamethibitika milele na milele. (Zab. 111:7, 8). Haiwezekani Mungu aliyeiumba sabato, akaona njema (Mwa.2:1-3 1:31) achague kuibadili. Jibu kwa swali ni kwamba Siye Mungu aliyebadili sabato.

Je ni Yesu? Yesu ni Bwana wa sabato (Mk.2:28) kwa kuwa aliiumba na kuitetea (Yoh.1:3, Kol. 1;16; Mk.2:27). Hakuja kuitangua torati wala manabii bali kutimiliza. (Mt. 5: 17, 18). Alipokuwapo duniani, ilikuwa desturi yake kuiheshimu. (Luk. 4:16) Kristo ni yuleyule jana na leo na hata milele (Ebr. 13.8). Katika kuilinda sabato, aliagiza wafuasi wake waombe mateso yasiwakute siku ya sabato. (Mt. 24:20). Katika maisha yake, Yesu aliiheshimu na hakutoa tamko kuihafifisha sabato. Jibu la swali ni kwamba hapana, Yesu hakubadili sabato.

Je, ni wanafunzi? Wanafunzi baada ya Yesu kufariki, waliharakisha mazishi yake yasifanyike siku ya sabato, na ilipofika sabato, pamoja na msiba, walistarehe kama ilivyoamriwa. (Luk. 23:54-56). Mitume walitumia siku za sabato kusali na kwa kushuhudia. (Mdo. 13: 14, 42-44 Mdo. 17:2, Mdo. 18:4). Kwa hiyo, siyo wanafunzi wa Yesu waliobadili sabato.

Kama siyo Mungu, Yesu au wanafunzi, ni nani basi? Hapa ndipo mwalimu wa Biblia anapopata shida kujibu swali. Kwa sababu kubadilishwa sabato kulifanyika nje ya Biblia, na wakati mwalimu anafundisha Biblia.

Kubadilishwa sabato kulifanyika pole pole lakini kwa uhakika. Wakristo walioishi Rumi hawakupenda desturi za Wayahudi, na kwa kuwa walitokana na wapagani waabudu jua, basi, waliona vema kukumbukia sikukuu zao za kizamani za kipagani. Hakuna mwandishi yeyote wa karne ya pili aliyetetea utakatifu wa Jumapili kutokana na Biblia. Siyo Barnabas, Ignatus, Justin, Iraneous, Tertullian wala Clement wa Rumi au Clement wa Alexandria au Victorinus au waandishi wengine aliyeishi karibu na nyakati za Yesu aliyejua kitu kama agizo la Yesu watu wasali siku ya kwanza ya Juma. Maxwell God's Care Vol. I.

Karne ya nne, mwaka 321 AD Konstatino Mkuu alitoa amri ya kutokufanya kazi siku ya Jumapili, na watu wangeweza kukutana kwa ibada siku hiyo. Miongo michache iliyofuata, mwaka 364 AD Baraza lililokaa Laodikia walitoa amri ya kwanza kikanisa watu waabudu siku ya Jumapili, na ikiwezekana, wasifanye kazi siku hiyo. Mwaka 538 AD, mwaka wa kwanza wa kuanza kuhesabu miaka 1260 ya utawala wa kanisa kwa uovu, Kanisa Katoliki katika Baraza lililoketi Orleans lilitoa amri ngumu zaidi kuliko ya Konstantino kwamba kazi za kilimo ziachwe Jumapili ili watu wapate fursa kwenda kuabudu.

Matamko ya Kanisa Katoliki yanakubali kwamba ndilo lililobadili sabato kutoka Jumamosi hadi Jumapili. James Kadinali Gibbons alipata kuandika, "Utasoma Biblia yote kutoka Mwanzo hadi Ufunuo na hutapata mstari moja unaohalalisha utakatifu wa Jumapili.

Maandiko Matakatifu hufundisha hukazia ibada ya kutunza Jumamosi ambayo sisi Wakatoliki hatuitunzi". James Gibbons Faith of Our Fathers Toleo la 47 la Mwaka 1895. Toleo la Katekisimu ya Mwongofu wa Kikatoliki la Mwaka 1977 ina maswali na majibu kama ifuatavyo:

Swali: Ni siku gani ndiyo Sabato?
Jibu: Jumamosi ndiyo Sabato
Swali: Kwa nini tunasali Jumapili badala ya Jumamosi?
Jibu: Tunasali Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki lilihamisha utakatifu kutoka Jumamosi hadi Jumapili.

Mwaka 1974 James Obrien alihitimisha vema juu ya mambo yahusuyo siku ya ibada. "Kwa kuwa Jumamosi siyo Jumapili imekaziwa katika Biblia, hatuoni ni jambo la kushangaza kwamba wasio wakatoliki huabudu Jumapili badala ya Jumamosi? Ndiyo, hakika. Destruri ya kusali Jumapili inatokana namamlaka ya Kanisa Katoliki. Kwa wasio wakatoliki wanaposali siku ya Jumapili, hiyo huwakumbusha mama yao walikotoka, sawasawa na mtoto aliyekimbia kwamba hamtaki mama yake, huku amebeba picha yake na akijificha, anaichukua anaitazama na kusema: mama yangu mzuri!

***Mabadiliko yalitabiriwa*.** Biblia inadokeza kwamba kutunza Jumapili kama siku ya ibada kumeanza na siri ya kuasi (2 Thes. 2:7). Danieli alisema mamlaka husika itatesa watu wa Mungu na kuazimu kubadili majira na sheria. (Dan. 7:25). Hata hivyo, mwisho wa mamlaka hiyo ni kushindwa (Dan. 7:11, 22, 26.) Mamlaka hiyo inatafsiri moja tu, nayo ni utawala wa Kanisa Katoliki.

Wakatoliki ndio wanaodai walibadilisha siku ya ibada kutoka Jumamosi hadi Jumapili. Zingatia Wasabato hawasemi Wakatoliki walibadili bali Wakatoliki wanadai kubadili. Juu ya wanaoacha kufuata kweli kwa kukumbuka siku isiyo katika amri takatifu, Mungu anasema Ibada yao ni bure (Mt. 15:8, 9). Zaidi ya hayo, sabato ya uwongo kwa kuwa haikuamriwa na Mungu itaondolewa (Mt. 15:13). Naam, katika mbingu mpya na nchi mpya wanadamu wote wataabudu siku ya Sabato. (Isa.66:22, 23.)

Matengenezo ya Sabato

Je, Sabato itarejeshwa tena? Jibu kwa swali hili ni ndiyo. Watu watajenga mahali palipobomoka na kutoihalifu sabato (Isa. 58:12-14). Katika kupeleka injili iletayo wokovu kwa wanadamu, imetolewa ahadi kwamba amebarikiwa ashikaye sabato. "BWANA asema hivi, Shikeni hukumu mkatende haki; kwa maana wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa. Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye sabato asizivunje, …wanaozishika sabato zangu nitawapa hawa …kumbukumbu na jina… (Isa. 56:1-8).

Kutangazwa kwa ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12 kutarejeza sheria ya Mungu. Wito wa kumcha Mungu na kumtukuza, unaelezea kuwa "Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na chemichemi za maji (Uf.14;7). Hili linarejea moja kwa moja amri ya nne inayohusu kuikumbuka sabato. Ujumbe wa malaika wa tatu utatengeneza watu wanaotii amri za Mungu na watakaokataa, watapokea alama ya mnyama (Uf.14:12, 9) na kukabiliwa na ghadhabu ya Mungu (Yoh.3:36).

Sababu za Uwongo zinazotumiwa na Wanadamu kuhafifisha Sabato

1. Je, tuheshimu Jumapili kwa kuwa Yesu alifufuka siku hiyo?

Hapana. Ni kweli baadhi ya wakristo wa awali kwenye miaka ya 90 hadi 100 BK walichagua kupumzika Jumapili kuepuka mateso makali yaliyowatofautisha na watu wengine. Hata hivyo Yesu anadai Je, tukatae amri ya Mungu kwa kuheshimu mapokeo? Wanafunzi waliokutana Jumapili wengi hawakuamini kama Yesu amefufuka (Mk. 16:12-14). Zaidi ya yote, mkutano wao wa Jumapili ulikuwa kwa hofu ya Wayahudi (Yoh. 20:19). Yako maadhimisho mengine muhimu kama ubatizo na meza ya Bwana je na hayo tuyawekee siku gani?

2. Je, si kalenda imebadilishwa?

Ni kweli kalenda ilibadilishwa mwaka 1582 lakini haikuingilia mzunguko wa juma lenye siku saba. Kilichobadilishwa na Papa Gregory XIII kilikuwa kusahihisha kosa kwenye kalenda ya Julian (46 BC) iliyosema mwaka una siku 365¼. Kwa uhalisia kuna dakika 11 pungufu katika hesabu hiyo. Hadi mwaka 1582, kulikuwa na upungufu wa siku 10. Hivyo, mwaka 1582 kulikucha Alhamisi 4 Oktoba 1582 na kesho yake kukawa Ijumaa tarehe 15 Oktoba 1582. Tunapoabudu siku ya sabato tunafanya kama Yesu alivyoabudu. (Luka 4:16.)

3. Ni vigumu kutambua ni siku ipi ndiyo ya saba katika wiki.

Ziko sababu mbili kuhusiana na jambo hili. Kwanza ni siku aliyokufa Yesu Luka 23:52-56 kwamba alikufa Ijumaa na alifufuka Jumapili. (Luka 24:1 – 2). Pili ni majina ya siku ya Jumamosi katika lugha mbali mbali zaidi ya 100 bado ni sabato. Italia, siku ya Jumamosi ni Sabbato, Hispania ni Sabado, Ureno ni Sabbado, Urusi ni Subbota, Poland ni Sobota na Ugiriki ni Sabbatho. Maana ya majina yote hayo ni kwamba Jumamosi ndiyo sabato. Ikiwepo hoja ya tatu basi ni Kamusi. Ukisoma Kamusi, neno sabato, ni siku ya saba ya juma kwetu ni Jumamosi.

4. Je naweza kutunza siku yoyote katika juma na kuiita Sabato?

La: Law. 10:1-2. Wana wa Haruni walipoleta moto wa kigeni kwenye madhabahu, waliangamizwa papo hapo. Hivyo, ni lazima kutakasa siku aliyoiweka Bwana mwenyewe. (Kut. 20: 10.) Zaidi ya yote, ukivunja amri moja, umekosa juu ya yote. Yak. 2:10. Kwa miaka 40 yaani zaidi ya sabato 2000, Mungu aliwafundisha Israeli Sabato. (Kut. 16.) Kuokota siku 6, sabato hakipatikani na Ijumaa kiliokotwa kikahifadhiwa pasipo kuharibika.

5. Tutaitakasa siku ya Bwana, achana na Sabato

Ufunuo 1:9, 10 hutambulisha siku ya Bwana. Siku za Bwana ziko nyingi. Malaki 4:1, 5 husema juu ya aina mojawapo na Isaya 58:13 husema juu ya Sabato. Yesu alisema ndiye Bwana wa Sabato. (Mk. 2:28.). Siku ya sabato humtambulisha Mungu kuwa Muumbaji na mkombozi na ndio maana uzito umewekwa kwamba tuikumbuke siku ya sabato tuitakase. (Kut.20:8).

6. Sabato ilifanyika kwa ajili ya Wayahudi peke yao

Kuna uwongo wa kutisha ulioenea duniani kwamba sabato ni ya Wayahudi. Lakini ndani ya Biblia wazo hilo haliungwi mkono. Sabato inayoungwa mkono, ni sabato ya Bwana. Kut. 20:10, Ni kweli lipo sinagogi la Wayahudi. (Mdo10:22, 12:11, 10:39 na 14:1.) Lakini sabato ni ya Bwana Kut. 20:10, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu Mk. 2:27.

Hivyo, kila aliye mwanadamu, sabato ni kwa ajili yake. Luka ambaye hakuwa myahudi alitakasa sabato (Mdo. 16:13.) Na waongofu waliabudu siku ya Sabato (Mdo. 14:42 – 44).

7. Amri 10 zilibatilishwa ikiwemo sabato

Inaumiza moyo kwamba wako watu wanaolisema jambo hili pasipo kuungwa mkono na Maandiko Matakatifu. Paulo anasema, kama isingekuwapo sheria, pasingekuwa na dhambi wala kusingekuwepo haja ya mwokozi. Rum. 4:15. Sheria ya Mungu yote, pamoja na sabato ni ya haki, takatifu na njema Rum. 7:12. Sheria ya Mungu huwakilisha tabia ya Mungu.

Rum 16:26 Mungu wa milele Zab. 111: 7,8 Sheria ni ya milele	Luk.18:19 Mungu ni mwema Rum. 7:12 Sheria ni njema
Yoh. 4:24 Mungu ni wa kiroho Rum.7:14 Sheria ni ya kiroho	Kumb. 32:4 Mungu ni wa haki Rum. 7:12 Sheria ni ya haki
Zab. 145:17 Mungu ni wa haki Zab.119:172 Sheria ni ya haki	1 Yoh. 3:3 Mungu ni safi Zab. 19:8 Sheria ni safi
Mt. 5:48 Mungu ni mkamilifu Zab. 19:7 Sheria ni kamilifu	1Yoh. 4:8 Mungu ni pendo Rum. 13:10 Sheria ni pendo
1 Yoh. 1:5 Mungu ni nuru Mith. 6:23 Sheria ni nuru	Zab. 48:1 Mungu ni mkuu Hos. 8:12 Sheria ni kuu
Kumb. 32:4 Mungu ni Kweli Zab. 119:142 Sheria ni kweli	Isa. 5:16 Mungu ni mtakatifu Rum. 7:12 Sheria ni takatifu

Kwa kuwa sheria ya Mungu ni mwakisio wa tabia ya Mungu, kwa kadiri tabia ya Mungu isivyobadilika, basi sheria nayo haitabadilika. Kama ingekuwa rahisi Mungu kubadilisha sheria yake, basi asingekubali Yesu kuja kufa msalabani kwa ajili ya wanadamu. Juu ya sheria ya Mungu kutofautiana na kile kinachoitwa Sheria ya Musa, Angalia somo la Sheria ya Mungu.

8. Sabato ilibatilishwa

Ni kweli yako mafungu ya Biblia yanayosema sabato ilibatilishwa. (Kol. 2:16, Gal. 4:10 and Rum 14:5) Biblia ikisomwa kwa makini itafunua kwamba hizi ni sabato zinazohusiana na sikukuu. Kufuatana na Mambo ya Walawi sura ya 23: angalia hasa fungu la 37, 38 kwamba zilitolewa kama nyongeza na ndio maana Paulo alizipinga. Tofauti na Sabato ya siku ya Saba, hiyo ilikuwapo kabla ya dhambi (Mwa.2:1-3). Mungu akaiweka kwenye sheria yake ya maadili yaani amri kumi (Kut.20:8-11). Ni alama ya Mungu kwa aliowaumba na kuwatakasa (Kut.31:17, 13; Eze.20:20, 12). Yesu alipokuwako duniani aliiheshimu. (Luk.4:16, Mt.24:20) na kwa kuwa Kristo habadiliki (Ebr.13;8), itakuwa furaha yake watakatifu kuabudu mbele zake siku za sabato, kwenye mbingu mpya na nchi mpya. (Isa.66:22, 23).

9. Tuko chini ya neema hivyo hatulazimiki kutii sheria Rum. 6:14 – 15,

Paulo anasema kwamba kwa kuwa chini ya neema, hatubatilishi sheria (Rum. 3: 31, Rum. 3:20.)

10. Tukiwa ndani ya Kristo, pumziko linatosha hivyo hatuihitaji sabato.

Ni Mungu ndiye atoaye raha hata kwa kupitia sabato yake. “Iko raha ya sabato kwa watu wa Mungu” (Ebr. 4:1-5, 9, 10). Jinsi wokovu ulivyo muhimu kwa mwanadamu, (Yoh. 3;16) ndivyo sabato ilivyo muhimu kwa wanadamu. (Mk.2:27)

11. Watu wengi hawawezi kuwa wamekosea

Wingi si hoja, bali ubora wa tabia ndio Mungu anaoutaka. (Mt. 7: 13, 14). Izingatiwe pia kwamba ilionywa kuwa watazuka watu wenye kufundisha kwa kufuata tamaa zao. (2 Timothy 4:3). Kwa hiyo kwa wingi wao, wanadamu wanaweza kukosea.

Namna ya Kuikumbuka Sabato na Kuitakasa

Kukumbuka na kuitakasa sabato ni kuelewa na kutekeleza kile ambacho Mungu anataka juu ya siku yake. Mungu hajatuacha juu ya mwongozo kwa jambo hili.

Kile Sabato inachofundisha kuhusu Mungu:

1. Mungu ni Mwumbaji (Mwa. 1 & 2 2:1 – 3). **2.** Mungu ni mkombozi na mwokozi atoshaye (Kut. 31:17, Eze. 20: 12, 20 Kumb. 5: 15) **3.** Mungu ni mweka maagano (Kut. 31:16, Kut. 19: 5,6. 1Pet. 2: 9, Uf. 1:6). **4.** Mungu ni mtoa karama njema na mtunzaji wa uumbaji (Mt. 5:45 Yoh. 5: 17) Uponyaji siku ya sabato humtambulisha Mungu mtunzaji (Yak. 1:17.). **5**. Mungu ni mkamilishaji (Ebr. 12:2, Isa. 66:22 Uf. 21: 1– 4.) **6.** Mungu hana upendeleo (Mdo. 10:34, Kut. 20:10) mtu, mke wake, watoto wake, wageni, watumwa kwa wajakazi wote wamepewa Sabato kwa kipimo sawasawa. **7**. Sabato hutambulisha Uungu wa Kristo (Mt. 12:8, Yoh. 5:17, 19, 20 Yoh. 9: 3- 5, Yoh. 10: 30).

Kile Sabato inachofundisha kuhusu Mwanadamu

1. Mwanadamu ni kiumbe. Hali hali ya kutokufa. Mungu pekee asiye na hali ya kutokufa (1Tim6: 16) atamrejesha mwanadamu kwenye uzima wa milele Kristo arudipo 1 Kor. 15: 51 – 54, 1Thes. 4:15 – 17. Katika hali yetu ya kuwa kiumbe, twapaswa kuwa wanyenyekevu. **2.** Sabato iko kwa wanadamu wote kwa kiasi sawa hata kwa mataifa Isa. 56;6, 7 Kut. 20:10. **3.**Thamani ya Mwanadamu kwa Mungu ni kubwa sana Mw. 1:31 cf 4, 12, 18, 21 25. Mwanadamu alipokosa, alimtuma Mwana wake wa pekee kuja kumwokoa. **4.** Hutufungamanisha kwa ushirika, upendo na kuhurumiana (kusanyiko takatifu Law. 23: 3). Kama Waisraeli walivyokuwa watumwa Misri, walipaswa nao kuwatendea kwa huruma mataifa mengine.

> "Taasisi takatifu ya Sabato ni ishara ya upendo wa Mungu kwa wanadamu. Ni ukumbusho wa uwezo wa Mungu katika uumbaji wa Mwanzo (Kut. 20:11) na dalili ya uwezo wake wa kuumba upya na kutakasa (Eze. 20:12), na utunzaji wake ni ushahidi wa utii wetu kwake (Uf. 14:12). Utunzaji sahihi wa Sabato ni ushahidi wa uaminifu wetu kwa Muumbaji wetu na wa ushirika wetu pamoja na Mkombozi wetu. Kwa maana ya pekee utunzaji wa Sabato ni kipimo cha utii. Tusipoweza kufaulu kipimo hicho, kama watu binafsi, tunawezaje kwa ukamilifu kutoa ujumbe wa Sabato kwa ulimwengu?" Kanuni za Kanisa (1995) Uk. 173.

Namna ya kuikumbuka Sabato na kuitakasa Kut. 20:8

Kuitakasa ni kuitendea kama kitu cha kicho, kuitenga kwa makusudi matakatifu (Eze. 20: 12). Kuikumbuka maana yake ni kuifikiria, kupangilia mambo kufanya ipendeze wakati wote wa wiki. (Kut. 20: 8 – 10). Kuangalia mtazamo wa sabato yaani siyo vema kuwaza mambo ya kazi katika Sabato (Amo. 8: 5). Ni siku ya furaha, kupendeza, twaacha mawazo yetu, maneno yetu na mahangaiko ya moyoni. (Isa. 58: 13). Hakuna kuuza wala kununua siku ya Sabato (Neh. 10: 31, 13: 15 – 22). Kuna kutaniko takatifu (Law. 23:3 Luk. 4: 16). Ni halali kutenda mema siku ya Sabato (Mt. 12:12).

Tunapokea kutoka kwa Yesu baraka ya ndani kabisa ya Sabato pumziko la kumwachia yeye mizigo yetu inayotuhangaisha. (Mt. 11: 28, 29, Ebr. 4: 4, 9, 10).

Kuangalia mapenzi ya Mungu: “Nifumbue macho yangu nipate kuona maajabu ya sheria yako”(Zab. 119: 18). Vitabu vitatu huimarisha Sabato: Biblia, Nyimbo, Uumbaji.

Maandalizi kwa ajili ya Sabato yapaswa kufanywa kwa juma lote. Hatupaswi kuishika Sabato kama jambo la kisheria tu bali twapaswa kutambua umuhimu wake kiroho. (Rum. 7:14, 6T353, 354). Pamoja na Sabato kuzingatiwa katika juma lote, Ijumaa ni siku maalum kwa maandalizi ya mwisho ya Sabato Luk. 23:54, 6T354

Kwa nuru iliyopo: -

Kazi zote siku ya Ijumaa jioni zapaswa kukoma (Kut. 20:10)

Tofauti zetu kati yetu na wanafamilia au washiriki wenzetu au hata majirani zapaswa kuondolewa (Yak. 5:16, Mt. 5: 23, 24)

Mapishi yapaswa kukamilika Ijumaa (Kut. 16:23 Luk. 23: 53-56) “Wakati mapishi yapaswa kuepukwa siku ya Sabato, siyo lazima kula chakula cha baridi. Nyakati za baridi, chakula kilichoandaliwa siku iliyopita kipashwe moto. Milo ipate kuwa miepesi yenye ladha nzuri na kuvutia. Andaa mlo ambao utaonekana tofauti na milo ya siku zingine.”(6T357).

“Saa za Sabato ni mali ya Mungu, na zitumiwe kwa ajili yake pekee. Anasa zetu wenyewe, maneno yetu wenyewe, shughuli zetu wenyewe, na mawazo yetu wenyewe, sipataiwe nafasi katika kuitunza siku ya Bwana. (Isa. 58:13). Hebu tujikusanye kando ya madhabahu ya familia wakati wa kuchwa kwa jua na kuikaribisha Sabato takatifu kwa maombi na nyimbo, na tuifunge siku hiyo kwa sala na maneno ya shukrani kwa ajili ya upendo wake wa ajabu.

“Sabato ni siku maalum kwa ibada nyumbani na kanisani, na siku ya kujifurahisha wenywe na watoto wetu, siku ambayo kwayo twaweza kujifunza zaidi juu ya Mungu kwa njia ya Biblia na kitabu cha somo kuu la viumbe asili. Ni wakati wa kuwazuru wagonjwa na kufanya kazi kwa wokovu war oho. Shughuli za siku sita za kufanya kazi ziwekwe kando. Kasi isiyo ya lazima isifanyike.

“Usomaji wa vitabu au magazeti ya kidunia au kusikiliza matangazo ya redio/televisheni visichukuwe muda wetu katika siku takatifu ya Bwana.

“Sabato haikusudiwi kuwa kipindi cha kutofanya chochote. Sheria hukataza kazi za kidunia katika siku ya pumziko la Bwana; kazi ya kujitaabisha iletayo riziki sharti ikome; kazi ya anasa za kidunia au za kupatia faida si halali katika siku hiyo; lakini kama vile Mungu alivyokomesha kazi zake za uumbaji, na akapumzika siku ya Sabato na kuibariki, vivyo hivyo mwanadamu ataacha shughuli za maisha yake ya kila siku, na kutoa hizo saa takatifu kwa pumziko la kiafya, kwa ibada, na kwa matendo matakatifu” Desire of Ages 207.

“Programu iliyoongozwa vizuri ya shughuli zinazowiana na roho ya utunzaji wa kweli wa Sabto itaifanya siku hii iliyobarikiwa iwe ya furaha sana na nzuri kuliko nyinginezo za juma, kwetu sisi na kwa watoto wetu, mwonjo halisi wa baadaye wa pumziko letu la mbinguni. Kanuni za Kanisa (1995) Uk. 174.

Safari na Sabato *Mdo 1:12*

Inashauriwa safari siku za Sabato ziepukwe kadiri inavyowezekana. Ikiwa ni lazima kusafiri siku ya Sabato, jipatie tiketi siku isiyo ya Sabato kabla ya kusafiri (6T360.)

Watumishi wa Hospitali na Sabato

Mara nyingi matabibu na wauguzi walio washiriki wetu huitwa siku ya Sabato kuhudumia wagonjwa na kuwalazimu kuacha mapumziko kuitikia miito ya kuhudumu. Mahitaji ya wanadamu wanaougua hayapaswi kupuuzwa.

Mwokozi kwa mfano wake mwenyewe amedhihirisha kwamba ni vema kusaidia kuondoa maumivu siku ya Sabato. Lakini shughuli isiyo lazima kama kuhudumia wagonjwa wa kawaida, kufanya operesheni isiyo lazima, ni vema vikaepukwa kufanywa siku ya Sabato 7T1
06.

Migahawa na Sabato

Je migahawa ifunguliwe siku ya Sabato? La, la. Kuishika siku ya Sabato kunatutambulisha sisi kuwa watu maalum wa Mungu. Alama hiyo haipaswi kuharibiwa. (7T121). Hata hivyo migahawa yaweza kuandaa chakula na kukifungasha vema ili wale wanaopenda wainunue Ijumaa jioni kwa kutumiwa siku ya Sabato 7T122)

Ili kuifanya Sabato takatifu, sisi wenyewe twapaswa kuwa watakatifu kwa kupokea haki ya
Kristo. Desire of Ages 283.